SHUGHULI ZA KISWAHILI KUSOMA KWA SAUTI - CBC GRADE 2 TERM 1 EXAMS 2023

MASWALI

1. Nitakusomea hadithi kisha nitakuuliza maswali. Sikiliza kwa makini.

Mwalimu ni mtu anayefunza wanafunzi. Mwalimu wetu anaitwa Bi. Aisha. Yeyeni mwalimu wa kike. Ana miaka thelathini na mitano. Mwalimu wetu ni mrefu. Yeye ni mnene. Rangi yake ni nyeusi. Wanafunzi wote wanampenda mwalimu wetu.

a. Mwalimu ni nani?
   (Mwanafunzi ajibu)
b. Mwalimu wetu anaitwa nani?
   (Mwanafunzi ajibu)
c. Yeye ana miaka mingapi?
   (Mwanafunzi ajibu)
d. Mwalimu wetu ana rangi gani?
   (Mwanafunzi ajibu)

2. KUSOMA KWA SAUTI (Alama 10)
Soma hadithi hii kwa sauti
Babu alitusimulia hadithi kuhusu lishe bora. Alituambia kuwa mihogo. mtama, maharagwe na viazi vitamu vinaongezea milli yetu nguvu. Alituambia tule matunda kama parachichi, papai, tufaha na mopera. Pia, alitueleza kuwa tuwe watoto ambao wanakula mboga kama vile minavu, mchicha na kabeji. Alitusisitizia kuwa mboga na matunda hukinga miili yetu dhidi ya magonjwa. Alimalizia kwa kusema lishe bora afya bora.